

## **DAWA YAKO: Glipizide \_\_\_\_ mg**

**Kwanini ninapatiwa dawa hii?** Una kisukari ama uko katika hatari ya kupata kisukari kwani una kiwango kikubwa sana cha sukari kwenye damu yako. Uwepo wa kiwango kikubwa sana cha sukari kwenye damu yako unaweza kusababisha mshtuko wa moyo, viharusi, ugonjwa wa figo, ama matatizo katika macho yako au mfumo wa neva.

**Ninakunywaje dawa hii:** Meza kidonge 1 kila siku, dakika 30 kabla ya kupata kifungua kinywa ama mlo wako wa kwanza wa siku. Jaribu kumeza kidonge hichi muda ule ule kila siku.

**Nitajihisije nitakapokunywa dawa hii?** Nyakati nyingine, huwa kuna athari za kimatibabu zinazotokana na kunywa dawa hii. Athari ya kimatibabu ni jambo lile unaloweza kujihisi ambalo si la kawaida. Baadhi ya athari za kimatibabu zinazotokana na kunywa Glipizide hutokea pindi mwili wako unapoanza kuizoea dawa hii na zinaweza kujumuisha kichefuchefu, kutapika, kuharisha na maumivu ya tumbo.

Baadhi ya athari za kimatibabu huwa hazitokei mara nyingi, hata hivyo zinaweza kuwa kali sana. **Piga 911 ama tembelea Chumba cha Dharura upesi iwapo utajihisi kupata: mabaka ya ngozi, kuvimba kwa uso, midomo, ulimi au koo; shida katika kupumua au kukosa pumzi AMA kupata mikazo ya misuli, udhaifu au kuchoshwa sana wakati wa mazoezi makali.**

### **Nini kingine ninachopaswa kufahamu?**

1. Unapaswa kunywa dawa hii kila siku hata pale utakapojihisi kuwa sawa.
2. Unapaswa kujaza upya dawa hii kila mwezi.
3. Kunywa maji mengi.
4. Unapaswa kumwona daktari kila baada ya miezi 3 ili kupima kiwango cha sukari kwenye damu yako.
5. Kama utatembelea ofisi ya daktari tofauti, kliniki tofauti ya kitabibu ama chumba tofauti cha dharura, utapaswa kuwataarifu kwamba una shinikizo la juu la damu na kwamba unakunywa dawa ya Glipizide.

“Maudhui haya ni ya kwa makusudi ya utoaji taarifa pekee na hayapaswi kuhesabiwa kuwa kama ushauri wa afya wa kitaalamu. Daima tafuta kupata ushauri kutoka kwa Tabibu wako ama mhudumu mwingine wa afya mwenye sifa, kuhusiana na maswali yoyote unayoweza kuwa nayo yanayohusu hali fulani ya kiafya au matibabu.”